




Tamara alikuwa msichana wa miaka mitano.

Aliishi na familia yake. Kijiji chao kilikuwa karibu na msitu wenye wanyama wakali.





Tamara aliwatii wazazi wake. Aliwasaidia kuwachunga kondoo na mbuzi wao.





Tamara alipenda kuwasikiliza ndege wakiimba. Ndege walipoimba, aliwaiga huku akitunga nyimbo zake.



Kwa sababu ya umri wake mdogo, Tamara hakuwa ameanza kwenda shule.

Nashipae na Tasioku walikwenda kwa sababu walikuwa wakubwa.





Nashipae, Tasiaku na watoto wengine kutoka kijijini walienda pamoja asubuhi na kurudi jioni. Walikuwa wakibeba chakula katika mikebe midogo.



Siku moja Tamara alimwuliza mamake, "Je, nitaanza kwenda shule lini?" Mama alimjibu, "Utaenda hivi karibuni mwanangu mpendwa."





Siku moja, chifu na wanawake wawili walifika nyumbani kwa gari. Lilikuwa jukumu la chifu kuhakikisha kwamba watoto wanaanza kwenda shule walipofikisha umri uliokubaliwa.



Watu waliamini kwamba mtoto akiweza kuunyoosha mkono wake kupita kichwani na kulishika sikio lake, mtoto huyo yuko tayari kuanza kwenda shule.





Chifu alimwuliza Tamara, "Una umri wa miaka mingapi?" Tamara alimjibu, "Mitano." "Hebu tuone ikiwa unaweza kwenda shule," chifu alisema.



Mmoja wa wanawake wale aliuchukuwa mkono wa kulia wa Tamara akauweka kichwani kwake. Tamara aliweza kulishika sikio lake la kushoto.





Waliamua kwamba wakati ulikuwa umefika wa Tamara kuanza kuhudhuria shule. Angeanza kwenda shule iliyokuwa karibu na nyumbani kwao.



Tamara alifurahi sana akawaza, "Nitajua kusoma na kuandika kama Nashipae na Tasieku wafanyavyo."